

Wasiliana na huduma ambazo zinaweza kukusaidia

Jinsi tunaweza kukusaidia

Watoto wanahitaji utulivu ili kuendelea na kukua kwa njia nzuri na bora, hata wakati familia zao zinakabiliwa na changamoto. Hii ni muhimu haswa katika miaka ya mapema ya mtoto.

Family and Child Connect inapatikana kwako ikiwa unahitaji usaidizi. Tunaweza kukuunganisha na huduma za eneo husika ili zikusaidie:

- kudhibiti tabia za mtoto wako
- kujenga mahusiano bora ya kifamilia
- kukomesha unyanyasaji nyumbani
- kupanga bajeti na kudhibiti pesa
- kudhibiti matatizo ya ulevi, dawa za kulevyu au kamari
- kupata makazi, huduma za afya au huduma nyingine za jamii au serikali.

Huduma za Family and Child Connect hutolewa na mashirika ya kuaminika, ya karibu ambayo yana uzoefu wa kushirikiana na familia.

Unaweza kutumia huduma hii mara nyingi kadiri unavyoihitaji.

Hakuna kikomo na hakuna gharama.

Nini kinafanyika unapowasiliana nasi?

Unapowasiliana nasi utazungumza na mfanyakazi mwenye uzoefu wa kutoa usaidizi kwa familia ambaye atasikiliza wasiwasi wako na kutathmini hali ya familia yako. Kila familia ni tofauti kwa hivyo, unapozungumza nasi, utapata ushauri na usaidizi mahususi kwa hali yako.

Tunaweza kukusaidia kwa simu moja tu, iwe kwa kutoa ushauri au kukuelekeza kwa huduma ya usaidizi. Tunaweza pia kupanga kukutembelea nyumbani kwako – au mahali salama – ili kuzungumza. Wakati inahitajika, tunaweza kuunganisha familia haraka na huduma za unyanyasaji wa nyumbani na familia.

Jinsi unaweza kuwasaidia wengine

Je, una wasiwasi kuhusu mtu mwengine, kama vile vijana wako, wajukuu, familia shulenii au rafiki kazini? Unaweza pia kuwasaidia kupata usaidizi wanaohitaji.

Anzisha mazungumzo nao na uwahimize wawasiliane na Family and Child Connect kwenye **13 32 64** kwa ushauri na usaidizi. Inaweza kuwa hatua yao ya kwanza kupata usaidizi wanaohitaji.

Wasiliana nasi

Watoto hustawi wakati wazazi wao wana usaidizi wanaohitaji. Katika Family and Child Connect, tunajua kwamba kuititia mwongozo unaofaa unaweza kukabiliana na changamoto za maisha na kusaidia watoto wako kukua kwa njia nzuri na bora.

Huduma yetu ni ya siri, ya bila malipo na yenye manufaa.

Simu: 13 32 64

Tovuti: familychildconnect.org.au

Huduma ya eneo lako ya Family and Child Connect ni:



Je, unahitaji mkalimani?

Ikiwa unahitaji mkalimani, tunaweza kupanga kuwa na mmoja bila malipo. Tupigie simu kwenye **13 32 64** na utueleze huduma ya lugha unayohitaji.